

Miundo ya Vishiriki vya Kitenzi Isiyofuata Udarajia wa Dhima za Kisemantiki katika Sentensi za Kiswahili

*Oliva Mang'ita*¹
Chuo Kikuu cha Dodoma
na

*Fabiola Hassan*²
Chuo Kikuu cha Dodoma

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.5>

Ikisiri

Makala haya yanahusu miundo ya vishiriki vya kitenzi isiyofuata Udarajia wa Dhima za Kisemantiki katika sentensi za Kiswahili. Msingi wake ni ukiukwaji wa Udarajia wa Dhima za Kisemantiki katika miundo ya vishiriki vya kitenzi katika sentensi za Kiswahili. Kwa mujibu wa udarajia, dhima za kisemantiki zipo katika mpangilio kuanzia nafasi ya juu kuelekea nafasi ya chini kulingana na uwezo wa dhima husika kuwa kiima cha sentensi. Kwa mujibu wa mpangilio huo, dhima iliyopo katika nafasi ya juu (kushoto) inapaswa kuwa kiima kuliko dhima iliyopo katika nafasi ya chini kuelekea kulia. Hata hivyo, ipo miundo inayokiuka utaratibu huu. Katika miundo hiyo, kishiriki chenye dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya chini huhusishwa na kiima ilhali kuna vishiriki vyenye hadhi ya kuwa kiima. Makala haya yanafanua miundo inayokiuka udarajia katika sentensi za Kiswahili. Data zilipatikana kwa njia ya uchambuzi matini, hojaji na upimaji wa usahihi wa kisarufi. Uchanganuzi wa data umetumia misingi ya Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu ya Bresnan na Kaplan (1970). Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, katika Kiswahili, kuna miundo isiyofuata udarajia. Kutokana na matokeo haya, makala yanahitimisha kwamba ipo miundo isiyofuata udarajia. Katika miundo hiyo, kuna upandishaji hadhi wa dhima iliyopo katika nafasi ya chini katika udarajia.

1.0 Utangulizi

Udarajia wa Dhima za Kisemantiki (kuanzia sasa UDK) ni mpangilio wa dhima za kisemantiki³ kuanzia nafasi ya juu (kushoto) kuelekea nafasi ya chini (kulia)

¹ Barua pepe: olivaeniko@gmail.com

² Barua pepe: fabiola.hassan@udom.ac.tz

³ Dhima za kisemantiki ni uamilifu wa kisemantiki wa vishiriki vya kitenzi kinachounda sentensi (Fillmore, 1968; Bresnan na Kanerva, 1989; Givon, 2001; Kroeger, 2004; Mkude, 2005). Dhima hizo ni kama vile mtenda (mtendaji wa tendo), kiathirika (anayeathirika na tendo), mnufaika (anayenufaika na tendo), kithimu (anayehusishwa na mahali/anayehama sehemu moja kwenda nyingine/anayebadilisha umilikiwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine), kimahali (mahali panapohusishwa na tendo), kiala (kifaa cha kutendea tendo), mpokeaji (mpokeaji wa kithimu) na mhisi (anayepata hisia hasi au chanya).

kulingana na uwezo wa dhima husika kuwa kiima⁴ kuliko dhima nyingine (Bresnan na Kanerva, 1989). Uwezo wa dhima husika kuwa kiima huongezeka kadiri unavyoelekea kushoto na hupungua kadiri unavyoelekea kulia. Hivyo, dhima iliyopo kushoto ndiyo yenye uwezo mkubwa wa kuwa kiima kuliko ile iliyopo kulia. Kielelezo Na. 1 kinaonesha UDK kwa mujibu wa Bresnan na Kanerva (1989).

Mtenda=>Mnufaika=>Mpokeaji/Mhisi=>Ala=>Kithimu/Muathirika=>Kimahali
Kielelezo Na. 1: Udarajia wa Dhima za Kisemantiki

Chanzo: Bresnan na Kanerva (1989: 23)

Kielelezo Na. 1 kinaonesha udarajia wa dhima za kisemantiki wa Bresnan na Kanerva (1989). Kulingana na kielelezo hiki, kiambajengo chenye dhima iliyopo katika nafasi ya juu (kushoto) ndicho hupaswa kuwa kiima katika sentensi kuliko kiambajengo chenye dhima iliyopo katika nafasi ya chini (kulia). Kwa mfano, kama katika sentensi kuna mtenda na kiathirika, mtenda anapaswa kuwa kiima na sio kiathirika. Mfano Na. (1) unathibitisha hoja hii.

- (1) *The hooligans broke the car windows.* [Kiingereza]
 Wezi walivunja vioo vya gari. (Tafsiri yetu)
 Walivunja (T) <mtenda, kiathirika>
 Dhima za kisarufi kiima yambwa
 Viambajengo wezi vioo vya gari
Chanzo: Levin na Hovav (2006:15)


Mfano Na. (1) unaonesha uhusishaji wa dhima za kisemantiki na za kisarufi kwa mujibu wa UDK. Katika mfano huu, mtenda *wezi* amehusishwa na kiima na kiathirika *vioo vya gari* kimehusishwa na yambwa. Hii ni kwa sababu, katika Kielelezo Na. 1, mtenda anatokea katika nafasi ya juu na kiathirika kinatokea katika nafasi ya chini. Hivyo, katika muundo wa <mtenda, kiathirika>, uhusishaji wa mtenda na kiima umefuata udarajia.

Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi (kuanzia sasa MVK) ni muundo unaoonesha kwamba kitenzi kinaambatana na vishiriki vyenye dhima zipi za kisemantiki.

⁴ Kiima ni dhima ya kisarufi ambayo mara nyingi hutokea kabla ya kitenzi na kuukilia upatanisho wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima. Dhima ya kisarufi ni uamilifu wa kisarufi unaofanywa na kiambajengo cha sentensi. Dhima za kisarufi ni kiima, yambwa, yambwa₀, oblikyu₀ na chagizo.

Vishiriki vya kitenzi ni viambajengo vinavyotokana na kitenzi. Kwa kawaida, kuna viambajengo vya lazima na vya hiari. Viambajengo vya lazima vinachangia kukamilisha maana ya sentensi na haviwezi kuondolewa bila kuathiri maana ya sentensi. Kielelezo Na. 2a kinaonesha MVK wenye viambajengo vya lazima.

Fundi amepaka rangi ukutani.


Amepaka (T) <mtenda, kithimu, kimahali>

 Viambajengo Fundi rangi ukutani

Kielelezo Na. 2a: MVK wenye Viambajengo vya Lazima

Kielelezo Na. 2a kinaonesha muundo wa kitenzi *amepaka*. Muundo huo unaonesha kwamba kitenzi *amepaka* kina mtenda *Fundi*, kithimu *rangi* na kimahali *ukutani*. Viambajengo hivi ni vya lazima katika MVK.

Kwa upande mwingine, kuna viambajengo vya hiari. Viambajengo hivi vinaongeza taarifa za ziada ambazo zinaweza kuondolewa bila kuathiri maana ya sentensi. Taarifa hizo zinaweza kuwa namna, wakati na mahali pa utendekaji wa tendo. Kielelezo Na. 2b kinaonesha muundo wenye viambajengo vya lazima na vya hiari.

Ukutani pamepakwa rangi na fundi.

Pamepakwa (T) <kimahali, kithimu, (mtenda)>

 Viambajengo ukutani rangi fundi

Kielelezo Na. 2b: MVK wenye Viambajengo vya Lazima na vya Hiari

Kielelezo Na. 2b kinaonesha kwamba kitenzi *pamepakwa* kina kimahali *ukutani*, kithimu *rangi* na mtenda *fundi*. Aidha, kimahali na kithimu ni vishiriki vya lazima, lakini mtenda ni kishiriki cha hiari. Ni kishiriki cha hiari kwa sababu ya uambikaji wa kiambishi cha utendwa {-w-} katika kitenzi *pamepakwa*. Uambikaji huo umepunguza ulazima wa mtenda *fundi*. Hivyo, katika sentensi *ukutani pamepakwa rangi*, hakuna ulazima wa kumtaja mtenda. Kwa hiyo, mtenda katika tungo hii ni mshiriki wa hiari.

Dhana ya muundo wa vishiriki vya kitenzi inahusiana na udarajia wa dhima za kisemantiki. Maandiko tangulizi yamefafanua kuhusu UDK. Miongoni mwa mambo yaliyofafanuliwa ni pamoja na kuunda darajia na kueleza matumizi ya darajia hizo katika kubaini usahihi wa tungo katika lugha (Fillmore, 1968; Jackendoff, 1972; Gee, 1974; Dik, 1978; Bresnan na Kanerva, 1989; Mkude,

2005; Bader na Bayer, 2006; Bresnan na Pylkkanen, 2010; Carolina na wenzake, 2015). Kwa mfano, Bresnan na Kanerva (1989) wanaeleza kwamba UDK unatumika kuhusisha dhima za kisemantiki na za kisarufi kwamba dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya juu katika udarajia huo huhusishwa na dhima ya kisarufi ya kiima. Hivyo, kwa kutumia udarajia ni rahisi kujua kiambajengo gani ni kiima cha sentensi. Mfano Na. (1) hapo juu unathibitisha matumizi ya UDK katika kuhusisha dhima za kisemantiki na zile za kisarufi.

Licha ya kupendekezwa kwa darajia mbalimbali na kisha kufafanuliwa matumizi yake, Newmeyer (2002) na Levin na Hovav (2006) wanadai kwamba darajia mbalimbali zilizopo zinasailika. Hii ni kwa sababu hakuna utafiti unaothibitisha kwamba kuna udarajia ambao unafanya kazi kwa ufanisi. Naye Kasper (2008) anaeleza kwamba udarajia wa Jackendoff (1972) haufanyi kazi katika miundo yote ya vishiriki vya vitenzi katika Kijerumani. Vilevile, Emanuel (2022) anadai kwamba UDK ulioelezwa na Mkude (2005) unasailika katika baadhi ya MVK katika sentensi za Kiswahili. Katika baadhi ya miundo ya vishiriki vya kitenzi, dhima ya kisemantiki iliyoko katika nafasi ya chini huhusishwa na kiima ilhali katika tungo kuna dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya juu. Mfano Na. (2) unathibitisha hoja hii.

- (2) *Baiskeli*^{kiathirika} *i-me-osh-w-a* (*na babu*)^{mtenda}
 Kng9.baiskeli kk9.tmlf.osh.ktndw. kt (na Kng1.babu)
 ‘Baiskeli imeoshwa na babu.’

Chanzo: Emanuel (2021)

Mfano Na. (2) unaonesha kwamba kiathirika *baiskeli* ambacho kinatokea katika nafasi ya chini katika udarajia kinahusishwa na kiima ilhali kuna mtenda *babu* ambaye anatokea katika nafasi ya juu kwenye udarajia.

Licha ya kutolewa kwa hoja kwamba ipo miundo ya vishiriki vya kitenzi ambayo haifuati udarajia katika Kiswahili, bado haikuwa wazi kwamba miundo ipi ya vishiriki vya kitenzi haifuati UDK katika Kiswahili. Hivyo, makala imebainisha na kufafanua miundo ya vishiriki vya kitenzi isiyofuata UDK wa Bresnan na Kanerva (1989) katika sentensi za Kiswahili. Tumetumia udarajia huo kwa sababu uliundwa kwa lengo la kuchanganua miundo ya vishiriki vya kitenzi katika lugha za Kibantu, ikiwamo lugha ya Kiswahili. Data zilizotumika katika makala haya zilipatikana kwa kutumia methodolojia ya utafiti kama ilivyofafanuliwa katika sehemu 2.0.

2.0 Methodolojia ya Utafiti

Data zilizotumika katika makala haya zilikusanywa uwandani, katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma. Mbinu zilizotumika kukusanyia data ni

uchambuzi matini, hojaji na upimaji wa usahihi wa kisarufi. Data zilikusanywa kutoka kwenye nakala 5 za gazeti la *Nipashe* mwezi Mei, mwaka 2024, wanafunzi 5 na wahadhiri 2. Idadi hii imetumika kwa sababu ilitosha kutupatia data za makala haya. Mwaka 2024 umetumika ili kuwakilisha machapisho ya miaka mingine. Pia, tumetumia mwaka huu kwa kuwa nakala zake zilipatikana kwa urahisi.

Gazeti la *Nipashe* liliateuliwa dhidi ya gazeti la *Mwananchi* na *Mtanzania* yaliyopatikana maktaba. Maktaba ya Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ilitumika kwa sababu watafiti walilenga kupata gazeti la lugha ya Kiswahili. Pia, watafiti walitumia gazeti na si matini zingine kwa sababu tafiti tangulizi zilionesha kuwa magazeti haya hujumuisha mijadala na taarifa mbalimbali ambazo hujengwa na tungo zenye miundo tofautitofauti. Gazeti hilo lilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu rahisi ambapo watafiti waliandika majina ya magazeti haya katika vikaratasi vitatu tofautitofauti. Baada ya hapo, watafiti walimuomba mhudumu wa maktaba kuokota kikaratasi kimoja. Kwa kutumia njia hiyo, watafiti walipata jina la gazeti la *Nipashe*. Halikadhalika, katika kupata nakala 5 kutoka katika gazeti la *Nipashe*, watafiti waliandaa vijikaratasi vitano (5) ambapo kwenye kila kikaratasi kimoja waliandika jina la mwezi fulani kutoka Januari 2024 hadi Mei 2024. Tumetumia mwezi Januari hadi Mei kwa sababu data za utafiti huu zilikusanywa Juni 2024. Watafiti walivikunja vikaratasi hivyo na kuvichanganya kwa pamoja. Baada ya hapo mtafiti alimuomba mhudumu wa maktaba kuokota kikaratasi kimoja. Kwa kutumia mbinu hii watafiti waliweza kupata kikaratasi kimoja ambacho kiliandikwa Mei.

Baada ya hatua hiyo, watafiti waliandaa vijikaratasi ambavyo viliandikwa tarehe 1 hadi 31. Kwa maana hiyo, kila tarehe iliandikwa kwenye kipande chake cha karatasi. Hivyo, watafiti walikuwa na jumla ya vijikaratasi 31. Watafiti walivikunja vijikaratasi hivyo na kuvichanganya katika bakuli. Kisha, mtafiti mmoja aliokota vijikaratasi vitano (5) kutoka kwenye bakuli hilo. Mchakato huo uliwapatia watafiti vijikaratasi vitano vilivyowakilisha nakala 5 za mwezi Mei kutoka kwenye gazeti la *Nipashe*. Kwa hiyo, zilipatikana nakala za tarehe 3, 5, 16, 17 na 21. Nakala hizi zilitumika kupata data kwa kutumia njia ya uchambuzi matini.

Pia, watafiti walilenga wanafunzi wa Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili (SHASAKI), mwaka wa tatu, 2023/2024. Wanafunzi wenye sifa hiyo walitumika kwa sababu wana maarifa ya Sintaksia ya Kiswahili ambayo wamekuwa wakijifunza katika kozi zao kuanzia mwaka wa kwanza mpaka mwaka wa tatu. Pia, wanafunzi hawa wanatumia Kiswahili katika mawasiliano yao ya ufundishwaji na ujifunzaji. Katika kuwapata wanafunzi, mbinu ya usampulishaji nasibu rahisi ilitumika. Watafiti walipelekwa darasani na uongozi wa Idara ya Kiswahili, kisha kutambulishwa kwa wanafunzi wa mwaka wa tatu SHASAKI.

Baada ya hapo watafiti waliwaomba walio tayari kushiriki katika kutoa data za utafiti huu wanyooshe mikono. Walionyosha mikono walikuwa 30 kati ya wanafunzi 65 ya waliokuwamo darasani. Kwa kuwa utafiti ulikusudia kupata watoataarifa 5 tu, watafiti waliandaa vijikaratasi 5 vilivyoandikwa NDIYO NITASHIRIKI na vijikaratasi 25 vilivyoandikwa ASANTE KWA KUJITOLEA. Watafiti, walikunja vijikaratasi hivyo na kuvipitisha kwa watafitiwa vikiwa ndani ya bahasha. Kila mwanafunzi aliyenyoosha mkono alichukua kijikaratasi kimoja. Baada ya mchakato huo, watafiti walipata wanafunzi 5 tu ambao walitumika katika mchakato mzima wa kukusanya data. Wanafunzi walitumika kutupatia data kupitia njia ya hojaji.

Pia, watafiti walitumia mbinu ya usampulishaji lengwa wa mtajo ili kupata wahadhiri 2. Katika njia hii, watafiti walienda kwa Mkuu wa Idara ya Kiswahili na kisha kutajiwa mhadhiri wa kwanza mwenye sifa lengwa. Sifa hizo ni kufundisha kozi za Sintaksia ya Kiswahili na kutumia Kiswahili katika mawasiliano ya ufundishaji. Kwa hiyo, mhadhiri wa pili mwenye sifa lengwa alitajwa na mhadhiri wa kwanza. Wahadhiri hao 2 walitumika kupata data kwa kutumia mbinu ya upimaji wa usahihi wa kisarufi.

Katika mbinu ya uchambuzi matini, watafiti waliandaa mwongozo wa uchambuzi matini. Mwongozo huo uliwaongoza watafiti kusoma nakala 5 za gazeti, kubainisha sentensi mbalimbali na kisha kuchambua MVK ya sentensi hizo. Mbinu hii iliawezesha watafiti kupata MVK isiyofuata UDK.

Katika mbinu ya hojaji, watafiti waliandaa hojaji yenye sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na MVK yenye vishiriki viwili vyenye dhima mbalimbali za kisemantiki. Aidha, mwambatano na mpangilio wa dhima hizo ulitofautiana baina ya muundo mmoja na mingine. Kwa kila muundo, watafiti waliwaomba wanafunzi 5 watunge sentensi kwa kuzingatia mwambatano na mpangilio wa dhima za kisemantiki zilizomo. Sehemu B ilikuwa na MVK yenye vishiriki vitatu vyenye dhima mbalimbali za kisemantiki. Mwambatano na mpangilio wa dhima hizo ulitofautiana baina ya muundo mmoja na mingine. Kwa kila muundo, watafiti waliwaomba wanafunzi 5 watunge sentensi kwa kuzingatia mwambatano na mpangilio wa dhima za kisemantiki zilizomo. Baada ya uchambuzi wa data, watafiti walipata data kuhusu miundo ya vishiriki vya kitenzi isiyofuata udarajia wa dhima za kisemantiki kwa kuzingatia misingi ya SLA.

Katika mbinu ya upimaji wa usahihi wa kisarufi, watafiti waliandaa mwongozo wa upimaji wa usahihi wa kisarufi. Mwongozo huo ulilenga kuthibitisha usahihi wa kisarufi wa sentensi zilizotungwa na wanafunzi katika hojaji kwa kuzingatia mwambatano na mpangilio wa dhima za kisemantiki. Kwa kutumia mwongozo huo, watafiti waliwaomba wahadhiri 2 kueleza kama sentensi ni sahihi au si sahihi

kisarufi. Mbinu hii iliawezesha watafiti kupata data kuhusu miundo isiyofuata udarajia.

Baada ya kukusanya data kwa kutumia uchambuzi matini, hojaji na upimaji wa usahihi wa kisarufi; hatua za uchambuzi wa data zilikuwa kama ifuatavyo: watafiti walipanga miundo inayofuata udarajia na ile isiyofuata udarajia, kisha, walibainisha na kufafanua miundo ya vishiriki vya kitenzi ambayo haifuati UDK. Uchanganuzi na ufasiri wa miundo hiyo ulizingatia misingi ya Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu (kuanzia sasa SLA). Nadharia hii imefafanuliwa katika sehemu 3.0.

3.0 Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu

Hii ni nadharia iliyoasisiwa na Joan Bresnan na Ronald Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970. Nadharia hii ilitokana na dosari za mageuzi katika Sarufi Geuzi. Miongoni mwa dosari hizo ni kukosekana kwa ujumla wa kanuni za kimageuzi ambazo zinaweza kufanya kazi katika lugha zote. Woods (1970) alipendekeza kuwa ufafanuzi wa lugha lazima uzingatie uambajengo pamoja na uamilifu wa viambajengo vya tungo. Kwa hiyo, Bresnan na Kaplan (1982) walitumia mawazo ya Woods kuweka misingi ya nadharia hii.

Nadharia ya SLA ina misingi mikuu kadhaa. Msingi wa kwanza ni uchanganuzi wa sentensi katika kiwango kimoja cha sentensi. Msingi wa pili ni uchanganuzi wa sentensi kwa kutumia taarifa za kileksika na uamilifu wa viambajengo vya sentensi. Msingi wa tatu ni kwamba kuna mikabala minne ya uchanganuzi wa sentensi na kwamba mikabala miwili inaweza kuhusishwa katika uchanganuzi wa sentensi moja. Mikabala minne ya uchanganuzi wa sentensi ni Mkabala wa Miundo ya Viambajengo (MkMV), yaani mkabala unaochanganua miundo ya maneno, virai na sentensi; Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo (MkUV), yaani mkabala unaochanganua dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi; Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi (MkVK), yaani mkabala unaochanganua dhima za kisemantiki za vishiriki vya kitenzi na Mkabala wa Muundo wa Taarifa (MkMT), yaani mkabala unaochanganua aina za taarifa zinazowasiliswa na viambajengo vya sentensi katika mawasiliano. Kwa kuzingatia msingi huu kwamba mikabala miwili inaweza kuhusishwa katika uchanganuzi wa sentensi; tunaweza kuhusisha MkVK na MkUV, yaani kuhusisha dhima za kisemantiki na dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi. Kielelezo Na. 3 kinaonesha uhusishaji wa MkVK na MkUV.

Kitenzi (T)	<Dhima ya Kisemantiki A,	Dhima ya Kisemantiki B>
Dhima za Kisarufi	Dhima ya Kisarufi A	Dhima za Kisarufi B
Viambajengo	Kiambajengo A	Kiambajengo B

Kielelezo Na. 3: Uhusishaji wa MkVK na MkUV

Kielelezo Na. 3 kinaonesha uhusishaji wa MkVK na MkUV. Katika kielelezo hiki, dhima za kisemantiki zinaweza kuhusishwa na dhima za kisarufi. Matalani, unaweza kuhusisha dhima ya kisemantiki A na dhima ya kisarufi A. Pia, unaweza kuhusisha dhima ya kisemantiki B na dhima ya kisarufi B.

Kwa kuwa msingi wa tatu unaruhusu uhusishaji wa dhima za kisemantiki na zile za kisarufi, katika makala haya, tulitumia msingi huu kuchanganua na kufasiri data kuhusu MVK isiyofuata udarajia wa dhima za kisemantiki wa Bresnan na Kanerva (1989). Hii ni kwa sababu, katika uhusishaji wa dhima za kisemantiki na za kisarufi, tuliweza kujua dhima ipi ya kisemantiki katika MVK wa sentensi inahusishwa na dhima ya kisarufi ya kiima. Baada ya kujua dhima hiyo, tulifasiri kwa kuzingatia nafasi ya dhima ya kisemantiki iliyohusishwa na kiima katika udarajia wa dhima za kisemantiki. Kama dhima hiyo inatokea katika nafasi ya chini ilhali katika MVK kuna dhima nyingine ya kisemantiki inayotokea katika nafasi ya juu, basi muundo huo wa vishiriki haufuati UDK. Kwa ujumla, misingi ya nadharia ya SLA, imetumika kuchanganua na kufasiri data zilizotumika katika makala haya. Data hizo zimetuwezesha kubainisha na kufafanua miundo isiyofuata udarajia katika sentensi za Kiswahili. Miundo hiyo imebainishwa na kufafanuliwa katika sehemu 4.0.

4.0 Miundo ya Vishiriki vya Kitenzi Isiyofuata UDK katika Sentensi za Kiswahili

Kwa mujibu wa data zilizochanganuliwa na kufasiriwa kwa kutumia nadharia ya SLA, ilibainika kwamba katika sentensi za Kiswahili kuna miundo tisa (9) ya vishiriki vya kitenzi ambayo haifuati UDK. Miundo hiyo ni <kimahali, kithimu, (mtenda)>, <kiala, (mtenda)>, <kimahali, kithimu>, <kiathirika, (mtenda)>, <mhisi, (mtenda)>, <kiathirika, kiala, (mtenda)>, <kithimu, kimahali, (mtenda)>, <mtenda & kiathirika>, pamoja na <mtenda & kiathirika/mnufaika>.

Kwa kuongezea, kulingana na tafiti tangulizi, miundo inayofuata UDK ni miundo wa vishiriki vya kitenzi unaoanza na mtenda, miundo wa vishiriki vya kitenzi unaoanza na mnufaika, miundo wa vishiriki vya kitenzi unaoanza na mpokeaji, miundo wa vishiriki vya kitenzi unaoanza na mhisi, miundo wa vishiriki vya kitenzi unaoanza na ala/kifaa, miundo wa vishiriki vya kitenzi unaoanza na kithimu, miundo wa vishiriki vya kitenzi unaoanza na kiathirika na miundo wa

vishiriki vya kitenzi unaoanza na kimahali. Ubainishaji wa miundo hii umezingatia kiambajengo chenye hadhi ya juu katika UDK. Kwa hiyo, kila muundo una miundo mingine ndani yake. Kwa ufupi, tumebainisha miundo hii ili kuwasaidia wasomaji kuweza kutambua miundo ya vishiriki vya kitenzi inayofuata UDK katika Kiswahili. Miundo inayokiuka UDK inafafanuliwa katika sehemu 4.1 – 4.8.

4.1 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi wenye <Kimahali, Kithimu, (Mtenda)>

Huu ni muundo wa vishiriki vya kitenzi unaounda sentensi zinazoanza na kimahali kabla ya kitenzi, kisha kufuatiwa na kithimu na mtenda wa hiari baada ya kitenzi. Kisintaksia, kimahali hutokea mwanzoni mwa sentensi na huukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima kk16 {*pa-*}, kk17 {*ku-*} au kk18 {*mu-*}. Kimofolojia, vitenzi vinavyounda tungo hizi huwa vimeambikwa kiambishi cha utendwa {-*w-*}. Kutokana na uambikaji wa kiambishi hicho, mtenda hushushwa hadhi na kuwa wa hiari katika sentensi. Jedwali Na. 1 linaonesha mifano ya sentensi inayoundwa na muundo huu wa vishiriki.

Jedwali Na. 1: Sentensi zenye MVK wa <Kimahali, Kithimu, (Mtenda)>

Na.	Kitenzi	Kimahali	Kithimu	Mtenda wa Hiari	Sentensi
1.	pambwa	ukumbini	maua	mpambaji	Ukumbini mumepambwa maua (na mpambaji).
2.	chomwa	msituni	moto	majangili	Msituni kumechomwa moto (na majangili).
3.	pakwa	ukutani	rangi	fundirangi	Ukutani pamepakwa rangi (na fundirangi).

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 1 linaonesha sentensi zenye MVK wa <kimahali, kithimu, (mtenda)>. Kisintaksia, vimahali *ukumbini*, *msituni* na *ukutani* vimetokea mwanzoni mwa sentensi na kuukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima, yaani kk18 {*mu-*}, kk17 {*ku-*} na kk16 {*pa-*} mtawalia. Kulingana na Nadharia ya SLA, tungo hizi hazifuata UDK kwa sababu kimahali ambacho kinatokea katika nafasi ya chini katika udarajia wa dhima za kisemantiki kinahusishwa na kiima ilhali kuna mtenda katika MVK. Kielelezo Na. 4 kinathibitisha hoja hii.

Ukumbini mumepambwa maua na mpambaji.

Mmepambwa (T)	<Kimahali,	Kithimu	(Mtenda)>	Dhima za Kisemantiki
	↓	↓	↓	
Dhima za Kisarufi	Kiima	Yambwa _θ	Chagizo	
	↓	↓	↓	
Viambajengo	ukumbini	maua	mpambaji	

Kielelezo Na. 4: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi yenye <Kimahali, Kithimu, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 4 kinaonesha kwamba kimahali *ukumbini* kinahusishwa na kiima na kithimu *maua* kinahusishwa na yambwa_θ. Kutokana na uambikaji wa kiambishi cha utendwa {-w-}, mtenda *mpambaji* ameshushwa hadhi na kuwa chagizo. Katika UDK, mtenda yupo katika nafasi ya juu na hivyo anapaswa kuwa kiima ikilinganishwa na kimahali. Hivyo, uhusishaji wa kimahali *ukumbini* na dhima ya kiima ni ukiukaji wa UDK. Kwa mujibu wa nadharia ya SLA, kimahali *ukumbini* ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *mumepambwa* kwa kutumia kk18 {mu-}. Kielelezo Na. 5 kinaonesha dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi pamoja na sifa zake za kimofosintaksia.

Ukumbini mumepambwa maua na mpambaji.

Kiima	PREDI	ukumbini
	kng	18
	ktm	ni
Kitenzi	mumepambwa <kimahali, kithimu, (mtenda)> <kiima, yambwa _θ , (chagizo)>	
	kk18	mu
	knj	me
	mz	pamb
	ktndw	w
	kt	a
Yambwa _θ	PREDI	maua
	kng6	ma
Chagizo	PREDI	(na mpambaji)

Kielelezo Na. 5: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kimahali, Kithimu, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 5 kinaonesha kwamba kimahali *ukumbini* ni kiima cha sentensi. Aidha, kimahali hiki kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *mumepambwa* kwa kutumia $kk18 \{mu-\}$. Pia, kithimu *maua* kinahusishwa na yambwa_θ na mtenda wa hiari *mpambaji* anahusishwa na chagizo. Kwa hiyo, MVK <kimahali, kithimu, (mtenda)> haifuati UDK kwa sababu kimahali ambacho kinatokea katika nafasi ya chini katika UDK kinahusishwa na kiima badala ya mtenda au kithimu.

4.2 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi wenye <Kiala, (Mtenda)>

Huu ni muundo wa sentensi zenye kiala na mtenda wa hiari. Kisintaksia, kiala hutokea kabla ya kitenzi na mtenda wa hiari hutokea baada ya kitenzi. Aidha, kiala huukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima. Kimofolojia, kitenzi kinachounda sentensi huwa kimeambikwa kiambishi cha utendwa katika kitenzi $\{-w-\}$. Kutokana na uambikaji wa kiambishi hicho, mtenda hushushwa hadhi na kufanywa kuwa wa hiari katika sentensi. Nao Mkude (2005) na Emanuel (2022) wanaeleza kuwa muundo wenye kiala na mtenda wa hiari huundwa na vitenzi elekezi vya utendwa ambavyo huwa na kiala na mtenda wa hiari. Jedwali Na. (2) linaonesha mifano ya sentensi zinazoundwa na MVK wa <kiala, (mtenda)>.


Jedwali Na. 2: Sentensi zenye MVK wenye <Kiala, (Mtenda)>

Na.	Kitenzi	Kiala	Mtenda wa Hiari	Sentensi
1.	imepikwa	sufuria	mpishi	Sufuria imepikiwa (na mpishi).
2.	imechorewa	kalamu	mchoraji	Kalamu imechorewa (na mchoraji).
3.	imeandikiwa	chaki	mwalimu	Chaki imeandikiwa (na mwalimu).

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 2 linaonesha tungo zenye MVK wenye <kiala, (mtenda). Kisintaksia, viala *sufuria*, *kalamu* na *chaki* vimetokea mwanzoni mwa sentensi na kuukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima $kk9 \{i-\}$. MVK ya tungo hizi haifuati UDK kwa sababu kiala ambacho kinatokea katika nafasi ya chini katika UDK kinahusishwa na kiima ilhali kuna mtenda. Kielelezo Na. 6 kinathibitisha hoja hii.

Sufuria imepikiwa na mpishi.




Kielelezo Na. 6: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kiala, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 6 kinaonesha kwamba kiala *sufuria* kinahusishwa na kiima. Kutokana na uambikaji wa kiambishi cha utendwa $\{-w-\}$, mtenda *mpishi* ameshushwa hadhi na kuhusishwa na chagizo. Kwa mujibu wa misingi ya nadharia ya SLA, hususani katika kanuni ya uhusishaji wa kimajumui wa dhima za kisemantiki na za kisarufi, kiala kinahusishwa na oblikyu_θ au kiima endapo MVK hauna kishiriki chenye hadhi zaidi ya kuwa kiima. Hivyo, MVK wa <kiala, (mtenda)> haufuati UDK kwani mtenda ndiye anapaswa kuwa kiima kuliko dhima nyingine.

Kwa mujibu wa nadharia ya SLA, kiala *sufuria* ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *imepikiwa* kwa kutumia kk9 $\{i-\}$. Kielelezo Na. 7 kinaonesha dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi pamoja na sifa zake za kimofosintaksia.

Sufuria inapikiwa na mpishi.



Kielelezo Na. 7: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kiala, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 7 kinaonesha kwamba kiala *sufuria* ni kiima cha sentensi. Aidha, kiala hiki kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *imepikiwa* kwa kutumia kk9 {i-}. Pia, mtenda wa hiari *mpishi* anahusishwa na chagizo. Kwa hiyo, MVK <kiala, (mtenda)> haufuati UDK kwa sababu kiala ambacho kinatokea katika nafasi ya chini katika UDK kinahusishwa na kiima badala ya mtenda.

4.3 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi wenye <Kimahali, Kithimu>

Huu ni muundo wa vishiriki vya kitenzi wa sentensi zenye upinduzi wa kimahali. Katika sentensi hizi kimahali hupandishwa hadhi na kutokea kabla ya kitenzi katika nafasi ya kiima. Wakati huohuo, kithimu, ambacho kinapaswa kutokea mwanzoni mwa sentensi katika nafasi ya kiima, hushushwa hadhi na kutokea baada ya kitenzi katika nafasi ya yambwa₀ (taz. Bresnan, 1994; Salzman, 2004 na Hassan, 2019). Jedwali Na. 3 linaonesha mifano ya sentensi zinazoundwa na MVK wa <kimahali, kithimu>.


Jedwali Na. 3: Sentensi zenye MVK wenye <Kimahali na Kithimu>

Na.	Kitenzi	Kimahali	Kithimu	Sentensi
1.	zagaa	mezani	maua	Mezani pamezagaa maua.
2.	jaa	shimoni	maji	Shimoni mumejaa maji.
3.	enea	Dodoma	habari	Dodoma kumeenea habari.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 3 linaonesha kwamba vimahali *mezani*, *shimoni* na *Dodoma* vimetokea mwanzoni mwa sentensi kabla ya vitenzi *pamezagaa*, *mumejaa* na *kumeenea* mtawalia. Aidha, vithimu *maua*, *maji* na *habari* vimetokea baada ya vitenzi hivyo. MVK wa <kimahali, kithimu> ambao unaunda tungo hizi haufuati UDK kwa sababu kimahali ambacho, kikilinganishwa na kithimu, kinatokea katika nafasi ya chini katika UDK kinapandishwa hadhi na kuhusishwa na kiima. Wakati huohuo, kithimu ambacho, kikilinganishwa na kimahali, kinatokea katika nafasi ya juu katika UDK kinashushwa hadhi na kuhusishwa na dhima ya kisarufi ya yambwa_θ. Kielelezo Na. 8 kinathibitisha hoja hii.


Shimoni mumejaa maji.



Kielelezo Na. 8: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kimahali, Kithimu>

Kielelezo Na. 8 kinaonesha kwamba kimahali *shimoni* ni kiima. Kwa upande mwingine, kithimu *maji* ni yambwa_θ. Kwa kuzingatia misingi ya nadharia ya SLA, kimahali *shimoni* ni kiima kwa sababu kinatokea kabla ya kitenzi *mumejaa* na kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi hicho kwa kutumia kk18 {*mu-*}. Aidha, kithimu *maji* ni yambwa_θ kwa sababu kinatokea baada ya kitenzi katika nafasi ya yambwa ingawa hakiwezi kuwa kiima cha sentensi tendwa (**Maji yamejawa na shimoni*). Kielelezo Na. 9 kinaonesha dhima za kisarufi na sifa za kimofosintaksia za viambajengo vya sentensi yenye MVK wa <kimahali, kithimu>.

Shimoni mumejaa maji.



Kielelezo Na. 9: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <kimahali, kithimu>

Kielelezo Na. 9 kinaonesha kwamba kimahali *shimoni* ni kiima. Kimahali hiki kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *mumejaa* kwa kutumia *kk18 {mu-}*. Pia, kithimu *maji* ni *yambwa_θ*. Hivyo, MVK wa <kimahali, kithimu> haufuati UDK kwa sababu kimahali ambacho kinatokea katika nafasi ya chini katika UDK kinahusishwa na kiima badala ya kithimu.

4.4 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi wenye <Kiathirika, (Mtenda)>

Huu ni muundo unaotokana na vitenzi vinavyoonesha athari ya tendo kwa mshiriki wa kitenzi. Kisintaksia, kiathirika hutokea kabla ya kitenzi na kisha kufuatiwa na mtenda baada ya kitenzi. Kimofolojia, vitenzi vinavyounda muundo huu huambikwa kiambishi cha utendwa {-w-}. Kutokana na uambikaji wa kiambishi hicho, mpangilio wa vishiriki vya kitenzi hubadilika kutoka ‘mtenda na kiathirika’ na kuwa ‘kiathirika na mtenda’ (taz. Mkude, 2005 na Emanuel, 2022). Pia, kiambishi hicho hushusha hadhi ya mtenda na kuwa mshiriki wa hiari kwa sababu anaweza kuondolewa au kubakizwa bila kuathiri maana ya sentensi. Jedwali Na. 4 linaonesha sentensi zinazoundwa na MVK wa <kiathirika, (mtenda)>.


Jedwali Na. 4: Sentensi zenye MVK wenye <Kiathirika, (Mtenda)>

Na.	Kitenzi	Kiathirika	Mtenda wa Hiari	Sentensi
1.	Daiwa	Waajiriwa 8000	Bodi ya Mikopo	Waajiriwa 8000 wanadaiwa (na Bodi ya Mikopo).
2.	Kamatwa	Viongozi wa CHADEMA	Jeshi la Polisi	Viongozi wa CHADEMA wamekamatwa (na Jeshi la Polisi).
3.	Vamiwa	Serikali ya Kenya	Wananchi	Serikali ya Kenya imevamiwa (na wananchi).

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 4 linaonesha kuwa viathirika *waajiriwa 8000*, *viongozi wa CHADEMA* na *serikali ya Kenya* vimetokea kabla ya vitenzi *daiwa*, *kamatwa* na *vamiwa* mtawalia. Watenda *Bodi ya Mikopo*, *Jeshi la Polisi* na *wananchi* wametokea baada ya kitenzi. Kimofolojia, vitenzi *daiwa*, *kamatwa* na *vamiwa* vimeambikwa kiambishi cha utendwa {-w-}. MVK wa <kiathirika, (mtenda)> haufuati UDK kwa sababu kiathirika ambacho kinatokea katika nafasi ya chini zaidi katika UDK, hupandishwa hadhi na kuhusishwa na kiima. Wakati huohuo, mtenda ambaye anatokea nafasi ya juu zaidi katika UDK, hushushwa hadhi na kuwa chagizo. Kielelezo Na. (10) kinaonesha uhusishaji wa dhima za kisemantiki na za kisarufi za viambajengo vya sentensi yenye MVK wa <kiathirika, (mtenda)>.

Waajiriwa 8000 wanadaiwa na Bodi ya Mikopo.




Kielelezo Na. 10: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kiathirika, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 10 kinaonesha kwamba kiathirika *waajiriwa 8000* kinahusishwa na kiima na mtenda wa hiari *Bodi ya Mikopo* anahusishwa na chagizo. Muundo huu haufuati UDK kwa sababu kiathirika kinatokea katika nafasi ya chini katika udarajia kuliko mtenda. Licha ya kutokea katika nafasi ya chini, anahusishwa na kiima. Tulitarajia mtenda ambaye anatokea katika nafasi ya juu katika UDK

ahusishwe na kiima, badala yake amehusishwa na chagizo. Kielelezo Na. 11 kinaonesha dhima za kisarufi na sifa za kimofosintaksia za viambajengo vya sentensi yenye muundo wa <kiathirika, (mtenda)>.

Waajiriwa 8000 wanadaiwa na Bodi ya Mikopo.



Kielelezo Na. 11: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kiathirika, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 11 kinaonesha kwamba kiathirika *waajiriwa 8000* ni kiima. Kiathirika hiki kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *wadaiwa* kwa kutumia *kk2* {*wa-*}. Pia, mtenda wa hiari *Bodi ya Mikopo* anahusishwa na chagizo. Kwa hiyo, muundo wa <kiathirika, (mtenda)> haufuati udarajia wa dhima za kisemantiki.

4.5 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi wenye <Mhisi, (Mtenda)>

Huu ni muundo unaotokana na vitenzi elekezi vya utambuzi au ufahamu. Kisintaksia, sentensi zenye muundo huu huanza na mhisi ambaye hutokea kabla ya kitenzi, kisha kufuatiwa na mtenda wa hiari baada ya kitenzi. Kimofolojia, vitenzi vinavyounda muundo huu huambikwa kiambishi cha utendesha kama vile {-ish/-esh/-sh/-z/-fy-} na kiambishi cha utendwa {-w-}. Kutokana na uambikaji wa kiambishi cha utendwa, mtenda hushushwa hadhi na kuwa wa hiari kwa sababu anaweza kuwapo au kuondolewa bila kuathiri maana ya sentensi. Jedwali Na. 5 linaonesha mifano ya sentensi zenye muundo wa <mhisi, (mtenda)>.

Jedwali Na. 5: Sentensi zenye MVK wenye <Mhisi, (Mtenda)>


Na.	Kitenzi	Mhisi	Mtenda	Sentensi
1.	Sikitishwa	ACT Wazalendo	Serikali	ACT Wazalendo imesikitishwa (na serikali).
2.	Furahishwa	Mwimbaji	Amapiano	Mwimbaji amefurahishwa (na Amapiano).
3.	Ogopeshwa	Mtoto	Simba	Mtoto anaogopeshwa (na simba).

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 5 linaonesha vishiriki ambavyo ni mhisi *ACT Wazalendo*, *mwimbaji* na *mtoto* vilivyotokea kabla ya vitenzi *sikitishwa*, *furahishwa* na *ogopeshwa* mtawalia. Aidha, mtenda *serikali*, *amapiano* na *simba* vimetokea baada ya vitenzi *sikitishwa*, *furahishwa* na *ogopeshwa* mtawalia. Aidha, hivi ni vitenzi tendeshwa ambavyo vina mwambatano wa kiambishi cha utendesha na kiambishi cha utendwa {-w-}. Uambikaji wa kiambishi cha utendwa {-w-} hufanya mtenda *serikali*, *amapiano* na *simba* kuwa viambajengo vya hiari.

Muundo wenye <mhisi, (mtenda)> haufuati udarajia kwa sababu mhisi ambaye anatokea katika nafasi ya chini katika udarajia anahusishwa na kiima ilhali mtenda ambaye anatokea katika nafasi ya juu kwenye udarajia anahusishwa na chagizo. Kielelezo Na. 12 kinaonesha uhusishaji wa dhima za kisemantiki na za kisarufi za viambajengo vya sentensi yenye muundo wa <mhisi, (mtenda)>.

Mwimbaji amefurahishwa na amapiano.




Kielelezo Na. 12: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wenye <Mhisi, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 12 kinaonesha kwamba mhisi *Mwimbaji* anahusishwa na dhima ya kisarufi ya kiima. Aidha, mtenda *amapiano* anahusishwa na dhima ya kisarufi ya chagizo. Mhisi ni kiima kwa sababu anaokulia upatanishi wa kisarufi na kitenzi. Anahusishwa na kiima badala ya mtenda kwa sababu ya athari za uambikaji wa kiambishi cha utendwa {-w-}. Hoja hii inaelezwa pia na Emanuel (2021) ambaye anasema kwamba mtenda anahusishwa na chagizo badala ya kiima kwa sababu ya

athari za kiambishi cha utendwa ambacho kinamshusha hadhi na kuwa kiambajengo cha hiari. Kielelezo Na. 13 kinaonesha dhima za kisarufi na sifa za kimofosintaksia za viambajengo vya sentensi yenye muundo wa <mhisi, (mtenda)>.

Mwimbaji amefurahishwa na amapiano.



Kielelezo Na. 13: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Mhisi, (mtenda)>

Kielelezo Na. 13 kinaonesha kwamba mhisi *mwimbaji* ni kiima cha sentensi. Aidha, mhisi huyu anakulia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *amefurahishwa* kwa kutumia *kk1* {*a-*}. Kitenzi *amefurahishwa* kimeambikwa kiambishi cha utendwa {-*w-*}. Kutokana na athari za kiambishi hicho, mtenda wa hiari *amapiano* anahusishwa na chagizo. Hivyo, MVK wa <mhisi, (mtenda)> haufuati udarajia.

4.6 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi wenye <Kiathirika, Kiala, (Mtenda)>

Huu ni muundo unaotokana na vitenzi elekezi vyenye <kiathirika, kiala na (mtenda)>. Kisintaksia, sentensi zenye muundo huu huanza na kiathirika ambacho hutokea kabla ya kitenzi, kisha hufuatiwa na kiala pamoja na mtenda wa hiari baada ya kitenzi. Aidha, kimofolojia, vitenzi vinavyounda sentensi hizi huambikwa kiambishi cha utendwa {-*w-*}. Kutokana na uambikaji wa kiambishi hicho, mtenda hushushwa hadhi na kuwa wa hiari kwa sababu anaweza kuondolewa bila kuathiri maana ya sentensi. Kwa upande mwingine, kiathirika

hupandishwa hadhi na kutokea katika nafasi ya kiima. Jedwali Na. 6 linaonesha sentensi za Kiswahili zenye muundo wenye <kiathirika, kiala, (mtenda)>.

Jedwali Na. 6: Sentensi zenye MVK wenye <Kiathirika, Ala, (Mtenda)>


Na.	Kitenzi	Kiathirika	Kiala	Mtenda wa Hiari	Sentensi
1.	limwa	shamba	jembe	mkulima	Shamba limelimwa kwa jembe (na mkulima).
2.	chapwa	kitabu	mashine	mchapishaji	Kitabu kimechapwa kwa mashine (na mchapishaji).
3.	letwa	mporaji	gari	polisi	Mporaji ameletwa kwa gari (na polisi).

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 6 linaonesha sentensi za Kiswahili ambazo viathirika *shamba*, *kitabu* na *mporaji* vimetokea mwanzoni mwa sentensi kabla ya vitenzi *limwa*, *chapwa* na *letwa* mtawalia. Vilevile, viala *jembe*, *mashine* na *gari* vimetokea baada ya vitenzi hivyo. Watenda *polisi*, *mchapishaji* na *mkulima* wametokea baada ya viala *jembe*, *mashine* na *gari* mtawalia. Kimofolojia, vitenzi *limwa*, *chapwa* na *letwa* vimeambikwa kiambishi cha utendwa {-w-}.

Tungo zenye <kiathirika, kiala, (mtenda)> hazifuati udarajia kwa sababu mtenda anapaswa kuwa kiima kuliko kiathirika, lakini katika muundo huu kiathirika kinapandishwa hadhi na kuwa kiima kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 14.


Shamba limelimwa kwa jembe na mkulima.



Kielelezo Na. 14: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi yenye Muundo wa <Kiathirika, Kiala, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 14 kinaonesha kwamba kiathirika *shamba* kinahusishwa na kiima, kiala *jembe* kinahusishwa na yambwa_θ na mtenda wa hiari *mkulima* ni chagizo. Uhusishaji wa kiathirika *shamba* na kiima unatokana na uambikaji wa kiambishi cha utendwa {-w-} ambapo kiathirika hicho kinapandishwa hadhi na kuwa kiima. Kwa upande mwingine, kiala *jembe* kinahusishwa na yambwa_θ na mtenda *mkulima* anashushwa hadhi na kuwa chagizo. Kiathirika *shamba* ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 15.

Shamba limelimwa kwa jembe na mkulima.



Kielelezo Na. 15: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kiathirika, Kiala, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 15 kinaonesha kwamba kiathirika *shamba* ni kiima. Kiathirika hiki kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *limelimwa* kwa kutumia kk5 {li-}. Kitenzi *limelimwa* kimeambikwa kiambishi cha utendwa {-w-} na hivyo mtenda wa hiari *mkulima* anahusishwa na chagizo. Kwa hiyo, muundo wa <kiathirika, kiala, (mtenda)> haufuati UDK.

4.7 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi wenye <Kithimu, Kimahali, (Mtenda)>

Huu ni muundo unaotokana na vitenzi elekezi vyenye kithimu, kimahali na mtenda wa hiari. Kisintaksia, sentensi zenye muundo huu huanza na kithimu ambacho

hutokea kabla ya kitenzi na kisha kufuatwa na kimahali na mtenda wa hiari baada ya kitenzi. Kimofolojia, sentensi hizo huundwa na vitenzi ambavyo vimeambikwa kiambishi cha utendwa {-w-}. Kutokana na uambikaji wa kiambishi cha utendwa, mtenda anashushwa hadhi na kuwa kiambajengo cha hiari. Jedwali Na. 7 linaonesha sentensi za Kiswahili zenye <kithimu, kimahali, (mtenda)>.

Jedwali Na. 7: Sentensi zenye MVK wenye <Kithimu, Kimahali, (Mtenda)>


Na.	Kitenzi	Kithimu	Kimahali	Mtenda wa Hiari	Sentensi
1.	letwa	zawadi	jimboni	mbunge	Zawadi imeletwa jimboni (na Mbunge).
2.	pelekwa	daftari	darasani	John	Daftari limepelekwa darasani (na John).
3.	pangwa	kuni	jikoni	wanafunzi	Kuni zimepangwa jikoni (na wanafunzi).

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 7 linaonesha kwamba vithimu *zawadi*, *daftari* na *kuni* vimetokea mwanzoni mwa sentensi kabla ya vitenzi *letwa*, *pelekwa* na *pangwa* mtawalia. Vitenzi hivyo vimefuatwa na vimahali *jimboni*, *darasani* na *jikoni* pamoja na watenda wa hiari *mbunge*, *John* na *wanafunzi*. Aidha, vitenzi *letwa*, *pelekwa* na *pangwa* vimeambikwa kiambishi cha utendwa {-w-}.

Muundo wenye <kithimu, kimahali, (mtenda)> haufuati kanuni ya udarajia kwa sababu mtenda anapaswa kuwa kiima kuliko kithimu, lakini katika muundo huu kithimu kimepandishwa hadhi na kuwa kiima kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 16.


Zawadi imeletwa jimboni na mbunge.



Kielelezo Na. 16: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi yenye Muundo wa <Kithimu, Kimahali, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 16 kinaonesha kuwa kithimu *zawadi* ni kiima, kimahali *jimboni* ni oblikyu_θ na mtenda wa hiari *mbunge* ni chagizo. Uhusishaji wa kithimu *zawadi* na dhima ya kiima unatokana na athari ya uambikaji wa kiambishi cha utendwa {-w-} ambapo kithimu *zawadi* kinapandishwa hadhi na kuwa kiima, kimahali *jimboni* kinahusishwa na oblikyu_θ na mtenda *mbunge* anashushwa hadhi na kuwa chagizo. Kithimu *zawadi* ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 17.

Zawadi imeletwa jimboni na mbunge.



Kielelezo Na. 17: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi yenye MVK wa <Kithimu, Kimahali, (Mtenda)>

Kielelezo Na. 17 kinaonesha kwamba kithimu *zawadi* ni kiima cha sentensi. Kithimu hiki kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *imeletwa* kwa kutumia kk9 {i-}. Kitenzi *imeletwa* kimeambikwa kiambishi cha utendwa {-w-}. Kutokana na athari za kiambishi hicho, mtenda wa hiari *mbunge* anahusishwa na chagizo. Aidha, kimahali *jimboni* kinahusishwa na oblikyu_θ. Hivyo, muundo wenye <kithimu, kimahali, (mtenda)> haufuati udarajia.

4.8 Miundo ya Vishiriki vya Kitenzi yenye <Mtenda & Kiathirika>

Huu ni muundo wa vishiriki vya kitenzi ambao unaundwa na kishiriki chenye dhima ya mtenda na kiathirika kwa wakati mmoja. Miundo hii inatokana na uambikaji wa kiambishi cha utendana {-an-} au cha ujirejeshi {-ji-}. Miundo hii imefafanuliwa katika sehemu 4.8.1 na 4.8.2.

4.8.1 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi Unaotokana na Kiambishi cha Utendana

Huu ni muundo unaotokana na uambikaji wa kiambishi cha utendana {-an-} katika kitenzi hisivu. Muundo huu unatokana na sentensi mbili ambapo kila sentensi inakuwa na mtenda na kiathirika, lakini kitenzi ni kilekile. Mtenda katika sentensi ya kwanza ni kiathirika katika sentensi ya pili na kiathirika katika sentensi ya kwanza ni mtenda katika sentensi ya pili. Kwa hiyo, uambikaji wa kiambishi cha utendana {-an-} katika kitenzi, huunganisha sentensi mbili, badala ya kuwa na vishiriki viwili, sentensi inakuwa na kishiriki kimoja chenye dhima ya mtenda na kiathirika kwa wakati mmoja kama inavyoonekana katika Jedwali Na. (8).

Jedwali Na. 8: Sentensi za Utendana zenye MVK wa <Mtenda & Kiathirika>


Na.	Kitenzi	Mtenda na Kiathirika	Sentensi
1.	pigana	Juma na John	i. Juma anampiga John. ii. John anampiga Juma = Juma na John wanapigana.
2.	shikana	Asha na Ally	i. Asha anamshika Ally. ii. Ally anamshika Asha. = Asha na Ally wanashikana.
3.	chekana	Rehema na Baraka	i. Rehema anamcheka Baraka. ii. Baraka anamcheka Rehema. = Rehema na Baraka wanachekana.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 8 linaonesha kwamba vishiriki *Juma na John*; *Asha na Ally* na *Rehema na Baraka* vina dhima ya mtenda na kiathirika kwa wakati mmoja.

Muundo wenye <mtenda & kiathirika> haufuati udarajia kwa sababu mtenda anapaswa kuwa kiima kuliko kiathirika, lakini katika muundo huu kiathirika kimepandishwa hadhi na kuwa kiima kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 18.


Juma na John wanapigana.



Kielelezo Na. 18: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi za Viambajengo vya Sentensi ya Utendana yenye MVK wa <Mtenda & Kiathirika>

Kielelezo Na. 18 kinaonesha kishiriki *Juma na John* kinahusishwa na dhima ya kisarufi ya kiima. Muundo huu unakiuka kanuni ya UDK kwa sababu kishiriki hiki kinabeba pia dhima ya kiathirika ambayo inatokea katika nafasi ya chini katika udarajia. Licha ya kutokea katika nafasi hiyo, kinahusishwa na kiima. Ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 19.

Juma na John wanapigana.



Kielelezo Na. 19: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo vya Sentensi ya Utendana yenye MVK wa <Mtenda & Kiathirika>

Kielelezo Na. 19 kinaonesha kwamba kiambajengo *Juma na John* ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *wanapigana* kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima *kk2 {wa-}*. Aidha, kitenzi *wanapigana* kimeambikwa kiambishi cha utendana *{-an-}*. Vilevile, kishiriki *Juma na John* kinakiuka UDK wa Bresnan na Kanerva (1989) kwa sababu katika udarajia huo,

hakuna dhima ya mtenda na kiathirika kwa wakati mmoja. Hivyo, muundo huu hauwezi kufafanuliwa na kanuni ya UDK.

4.8.2 Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi Unaotokana na Kiambishi cha Ujirejeshi

Huu ni muundo wa vishiriki vya kitenzi katika sentensi za ujirejeshi. Kimofolojia, vitenzi vinavyounda sentensi huambikwa kiambishi cha ujirejeshi {-ji-}. Kisemantiki, hizi ni tungo ambazo mtenda na muathirika/mnufaika ni yuleyule mmoja, yaani mtendaji na mtendwaji wa tendo ni yuleyule (taz. Hassan, 2021/2022). Jedwali Na. 9 linaonesha sentensi zenye kiambishi cha ujirejeshi zenye MVK wa <mtenda & kiathirika/mnufaika>.

Jedwali Na. 9: Sentensi zenye Ujirejeshi zenye MVK wa <Mtenda & Kiathirika/Mnufaika

Na.	Kitenzi	Mtenda na kiathirika/mnufaika	Sentensi
1.	jinyonga	mwanamke	Mwanamke _i ; amemnyonga mwanamke _i ; Mwanamke amejinyonga.
2.	jigonga	Juma	Juma _i ; amengonga Juma _i ; Juma amejigonga.
3.	remba	Asha	Asha _i ; amemremba Asha _i ; Asha amejiremba.

i – kirejelewa cha kiambajengo cha kwanza ni sawa na kirejelewa cha kiambajengo cha pili.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Jedwali Na. 9 linaonesha kwamba *mwanamke* na *Juma* ni vishiriki vyenye dhima ya mtenda na mwathirika kwa wakati mmoja. Vilevile, kiambajengo *Asha* ni kishiriki chenye dhima ya mtenda na mnufaika kwa wakati mmoja. MVK wa <mtenda & kiathirika/mnufaika> katika tungo za ujirejeshi haufuati UDK kwa sababu kishiriki chenye dhima mbili huhusishwa na kiima kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 20.

Mwanamke amejinyonga.

Amejinyonga (T) <Mtenda & Kiathirika> dhima za Kisemantiki

Dhima ya Kisarufi

Kiima


Kiambajengo

Mwanamke

Kielelezo Na. 20: Uhusishaji wa Dhima za Kisemantiki na ya Kisarufi ya Kiambajengo cha Sentensi ya Ujirejeshi yenye MVK wenye <Mtenda & Kiathirika>

Kielelezo Na. 20 kinaonesha kwamba kiambajengo *mwanamke* ni mtenda na kiathirika kwa wakati mmoja. Kiambajengo hiki kinahusishwa na kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 21.

Mwanamke amejinyonga.



Kielelezo Na. 21: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimfosintaksia za Viambajengo vya Sentensi ya Ujirejeshi yenye MVK wa <Mtenda & Kiathirika>

Kielelezo Na. 21 kinaonesha kwamba kiambajengo *mwanamke* ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *amejinyonga* kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima *kk1 {a-}*. Aidha, kitenzi *amejinyonga* kimeambikwa kiambishi cha ujirejeshi *{-ji-}*. Muundo wa <mtenda & kiathirika> katika sentensi za ujirejeshi unakiuka UDK kwa sababu kiambajengo *mwanamke* kinabeba pia dhima ya kiathirika ambayo inatokea katika nafasi ya chini katika UDK. Licha ya kutokea katika nafasi hiyo, kinahusishwa na dhima ya kiima. Pia, katika UDK, hakuna dhima ya mtenda na kiathirika/mnufaika kwa wakati mmoja. Hivyo, muundo huu hauwezi kufafanuliwa na kanuni ya UDK.

Kwa ujumla, sehemu 4.1 – 4.8 zimebainisha na kufafanua MVK isiyofuata UDK katika sentensi za Kiswahili. Katika miundo hii dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya chini katika UDK inapandisha hadhi na kuwa kiima ilhali kuna dhima nyingine za kisemantiki zinazopaswa kuwa kiima.

5.0 Hitimisho

Katika makala haya, tumebainisha na kufafanua MVK 9 isiyofuta UDK. Miundo hiyo ni <kimahali, kithimu, (mtenda)>, <kiala, (mtenda)>, <kimahali, kithimu>, <kiathirika, (mtenda)>, <mhisi, (mtenda)>, <kiathirika, kiala, (mtenda)>, <kithimu, kimahali, (mtenda)>, <mtenda & kiathirika> na <mtenda & kiathirika/mnufaika>. Katika miundo hii, kuna ushushaji hadhi wa dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya juu katika UDK. Kwa upande mwingine, kuna upandishaji hadhi wa dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya chini katika UDK. Hivyo, ni vyema ukafanyika utafiti wa kina ili kueleza sababu za jumla za ushushaji na upandishaji hadhi wa dhima za kisemantiki katika miundo yote ya vishiriki vya kitenzi ambayo haifuati udarajia katika mawasiliano. Hii itasaidia kuutumia UDK kwa hadhari huku tukizingatia sababu za kimawasiliano za ukiukaji wa UDK kwa wazungumzaji wa Kiswahili.

Vifupisho na alama zilizotumika:

kk	=	Kipatanishi cha Kiima
kng	=	Kiambishi cha Ngeli
knj	=	Kiambishi cha Njeo
kuj	=	Kiambishi cha Ujirejeshi
kt	=	Kiambishi Tamati
ktm	=	Kiambishi Tamati cha Mahali
ktndea	=	Kiambishi cha Utendea
ktndn	=	Kiambishi cha Utendana
ktndw	=	Kiambishi ya Utendwa
MkMT	=	Mkabala wa Muundo wa Taarifa
MkMV	=	Mkabala wa Miundo ya Viambajengo
MkUV	=	Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo
MkVK	=	Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi
MVK	=	Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi
mz	=	Mzizi
↓	=	Kinahusishwa na
*	=	Isiyosahihi Kisarufi
< >	=	Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi
< a, b >	=	MVK ambapo vishiriki vyote ni vya lazima
<a, (b) >	=	MVK ambapo kishiriki b ni cha hiari

Marejeleo

- Bader, M. na Bayer, J. (2006) *Case and Linking in Language Comprehension: Evidence from German*. Dordrecht: Springer.
- Bresnan, J. (1994) "Locative Inversion and Architecture of Universal Grammar". *Language*, Juz. Na. 70: 72-131.

- Bresnan, J. na Kanerva, J. (1989) "Locative Inversion in Chichewa: A Case Study of Factorization in Grammar". *Linguistic Inquiry*, Juz. 20(1): 1-50.
- Bresnan, J. na Kaplan, R. M. (1982) "Lexical-function Grammar: A Formal System for Grammatical Representation". Katika J. Bresnan (Mh.) *The Mental Representation of Grammatical Relations*. Cambridge: The MIT Press. kur. 173 – 281.
- Bresnan, L. na Pyllkanen, L. (2010) "Processing Psych Verbs: Behavioral and MEG Measure of Two Different Types of Semantic Complexity". *Language and Cognitive Processes*, Juz. 25(6): 777-807.
- Carolina, G., Wainelboim, J. A., Paris, L. na Michael, W. D. (2015) "The Thematic Hierarchy in Sentence Comprehension: A Study on the Interaction between Verb Class and Word Order in Spanish". *The Quarterly Journal of Experimental Psychology*, Juz. 68(10): 1-65.
- Dik, S. C. (1978) *Functional Grammar*. North-Holland: Amsterdam.
- Emanuel, F. (2021) "Dhima za Kisarufi na Kisemantiki za Viambajengo Vinavyohusika katika Uchanganuzi wa Tungo za Utendeka na Utendwa". *Mulika*, Juz. 40(1): 57-74.
- Emanuel, F. (2022) *Uchanganuzi wa Tungo za Utendeka na Utendwa katika Lugha ya Kiswahili*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.
- Fillmore, C. (1968) "The Case for Case". Katika E. Bach na R.T. Harms (Wah.) *Universal in Linguistic Theory*. New York: Holt Rinehart and Winston. kur. 1-90.
- Gee, J. P. (1974) "Jackendoff's Thematic Hierarchy Condition and the Passive Construction". *Linguistic Inquiry*, Juz. 5: 304-308.
- Givon, T. (2001) *Syntax: An Introduction*. Amsterdam/Philadelphia: John Bnejamins.
- Hassan, F. (2019) *Uchanganuzi wa Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Hassan, F. (2021) *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Hassan, F. (2022) *Sintaksia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Jackendoff, R. (1972) *Semantic Interpretation in Generative Grammar*. Cambridge: MIT Press.
- Kasper, S. (2008) *A Comparison of Thematic Role Theories*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). University of Marburg.
- Kroeger, P. R. (2004) *Analysing Syntax: A Lexical Functional Approach*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Levin, B. na Hovav, R. M. (2006) *Argument Realization*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mkude, D. J. (2005) *The Passive Construction in Swahili*. Tokyo: Research Institute for Language and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

- Newmeyer, F. (2002) "Optimality and Functionality: A Critique of Functionally-Based Optimality Theoretic Syntax". *Natural Language and Linguistic Theory*, Juz. 20: 43-80.
- Salzman, M. D. (2004) *Theoretical Approaches to Locative Inversion*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). University of Zurich, Zurich.
- Woods, W. A. (1970) "Transition Network Grammars for Natural Language Analysis". *Communications of the ACM*, Juz.13(10): 591-606.